

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
(FASIHI)
JULAI / AGOSTI 2009
MUDA: SAA 2^{1/2}

MITIHANI YA MAKADIRIO YA WILAYA YA BORABU - 2009
Kenya Certificate of Secondary Education (K.C.S.E)

102/3
KISWAHILI
KARATASI YA 3
(FASIHI)
MUDA: SAA 2 ½

MAAGIZO:

- Jibu maswali **manne** pekee.
- Swali la **kwanza** ni la **lazima**
- Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani:- Tamthilia, Riwaya, Hadithi fupi na Ushairi.
- Usijibu maswali **mawili** kutoka **sehemu moja**.

*Karatasi hii ina kurasa 4 zilizopigwa chapa, watahiniwa
lazima wahakikishe kurasa zote zimepigwa chapa
sawa sawa na kuwa maswali yote yamo.*

(LAZIMA) FASIHI SIMULIZI

1. a) Eleza maana ya vitendawili (alama2)
- b) Fafanua hatua tano za utegaji wa vitendawili (alama5)
- c) Eleza umuhimu wa vitendawili kwa jamii (alama4)
- d) Toa sifa bainifu za vitendawili (alama5)
- e) Taja aina nne za vitendawili ukizingatia lugha. (alama4)

RIWAYA

2. “Mabadiliko ni maumbile yenyewe. Kutokea kwa mabadiliko ni sheria na kanuni inayoendesha ulimwengu huu....”
 - a) Eleza muktadha wa dondoo hili. (alama 4)
 - b) Fafanua mabadiliko matano ambayo ameyapitia msemaji (alama10)
 - c) Eleza sifa sita za msemaji, huku ukitoa mifano mwafaka kutoka riwayani. (alama6)
3. Huku ukitoa mifano mwafaka, jadili jukumu la mwanamke katika riwaya ya utengano (alama20)

TAMTHILIA

KIFO KISIMANI – KITHAKA WA MBERIA

4. “Mara nyingi vijana hushughulikia mambo ya kibinafsi. Mara nyingi mawazo yao hufuata mkondo wa anasa za vijana tu.....”
 - a) Eleza muktadha wa dondoo hili (alama4)
 - b) Onyesha ushahidi wowote katika tamthilia kudhihirisha ukweli wa kauli hii (alama6)
 - c) Fafanua mambo matano waliyoyafanya vijana katika tamthilia kudhihirisha kuwa walipigana kwa niaba ya umma. (alama10)
5. Linganisha wasifu wa wahusika wafuatao na uonyeshe umuhimu wao katika tamthilia ya kifo Kisimani (alama20)
 - a) Bokoro
 - b) Mwelusi

HADITHI FUPI

K.W. WAMITILA – MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI ZINGINE

6. Onyesha jinsi mwanamke alivyosawiriwa katika hadithi za uteuzi wa moyoni na Ngome ya Nafsi (alama 20)

USHAIRI

7. Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata

- | | | |
|-----|---|---|
| 1. | Dharau ije kwa <i>bezo</i>
<i>Iwile</i> kama <i>fumizo</i>
Dharau ni angamizo | mtu kumkata pua
ghafula kuja muua
kwa wale wasotambua |
| | Mtu humkata pua! | |
| 2. | Dharau ije kwa <i>mzo</i>
Kwa ufanyae vikwazo
Kama vile mtelezo | mja humuangamiza
dharau ishakuweza
dharau hukubwatiza |
| | Mja humuangamiza! | |
| 3. | Dharau ni <i>mwambuzo</i>
Kipele cha mkwaruzo
Yazidipo matatizo | kidonda inaambuzi
machozi huja kuliza
mguu ukipoteza |
| | Kidonda inaambuzi! | |
| 4. | Dharau kwa kazi <i>twezo</i>
Haikupi kishikizo
Malipo yako na tuzo | hwenda ukaipoteza
wewe na kazi kucheza
kazini hukufukuza |
| | Hwenda ukaipoteza! | |
| 5. | Dharau mfwatilizo
Haiwi haiwi hizo
Dharau si ya <i>chetezo</i> | inangoja kumaliza
kuwa kutakutimiza
kinga haitapatiza |
| | Inangoja kumaliza! | |
| 6. | Dharau si <i>maliwazo</i>
Na nyakati zipitazo
Dharau ni <i>fumanizo</i> | kukaa 'kizungumza
wewe uli <i>ukichuza</i>
ghafila huja <i>kupaza</i> |
| | Dharau si maliwazo! | |
| 7. | Dharau ni <i>mabwagizo</i>
Hukuvunjia uwezo
Na mingi kwako <i>mizozo</i> | maisha kudidimiza
kutenda na kufanyiza
kote imekuzingiza |
| | Dharau ni mabwagizo! | |
| 8. | Dharau ni maapizo
Hupungukiwa mawazo
Muokwako <i>matutizo</i> | laana ya <i>kuapiza</i>
na watu hukupuza
na kuzama na <i>kuviza</i> |
| | Dharau ni maapizo! | |
| 9. | Dharau ni matelezo
Na hakuna <i>mazuizo</i>
Purr chini <i>kunasazo</i> | Chini <i>yatakubwagiza</i>
telezi ukiteleza
kuinuka hutaweza |
| | Dharau ni matelezo! | |
| 10. | Dharau ni hitimizo
Ninafunga beti hizo
Ikimbie ndugu guzo | wasia wangu chukua
kumi niloziambua
dharau <i>inaumbua</i> |
| | Dharau ni hitimizo! | |

(Kutoka: *Stadi za Lugha, Kitabu cha 3, Said A. Mohamed, OUP, uk. 31 – 32*)

Maswali:-

- | | | |
|----|--|----------|
| a) | Lipe shairi hili kichwa mwafaka | (alama1) |
| b) | Shairi hili ni la bahari gani. Toa sababu. | (alama2) |
| c) | Fafanua dhamira za shairi hili | (alama4) |

- d) Onyesha muundo wa shairi hili (alama5)
- e) Taja na ueleze tamthali tatu za lugha zilizotumika katika shairi hili (alama6)
- f) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi (alama2)
- i) fumanizo
- ii) mwambuzo